



UBISHI TUUU: HUU UTITIRI WA MASHANGINGI SIO UTHIBITISHO WA MAISHA BORA?SASA HIYO NI AWAMU YA KWANZA.AWAMU IJAYO NI BAJAJ KWA WAJAWAZITO NCHI NZIMA





**HATA SUPAMODO NAOMI CAMPBELL ALIPOTEMBELEZA TANZANIA
ALIRIDHISHWA NA HALI ALIYOKUTA WODI YA AKINAMAMA.NA AKATOA
MACHOZI YA FURAHIA**



YOU SEE, TATIZO LA MAJI MIJINI NA VIJIJINI LIMEPATIWA UFUMBUZI WA KUDUMU



**AKINAMAMA WAMEPEWA KIPAUMBELE CHA HALI YA JUU KATIKA MIPANGO
YA SERIKALI YA KIKWETE. PICHA INAWAONYESHA KAMA WANA MAJONZI
LAKINI UKWELI NI KUWA WAMESHIKWA NA BUTWAA KUTOKANA NA KAZI
NZURI YA CHAGUO LA MUNGU KIKWETE**








PICHA YA JUU NA YA CHINI: CHAGUO LA MUNGU DANCING.BY THE WAY "Never Trust a Spiritual Leader who cannot Dance".-Mr Miyagi,The Next Karate Kid,1994



**NDIO MAANA RAIS MPENDWA JAKAYA KIKWETE ALISEMA MIMBA ZA
WANAFUNZI NI KIMBELEMBELE CHAO TU. ANGALIA MWENYEWWE MAZINGIRA
BORA KABISA YA NAMNA VIJANA WETU WANAVYOPATA ELIMU. KIKWETE
OYEEE**



**SERIKALI YA KIKWETE IMEWAJALI SANA WANAFUNZI NA KUWANUNULIA
MADAWATI BORA MNO HADI YANAWACHOSHA KUYAKALIA NA KUAMUA
KUKAA SAKAFUNI**



USHAHIDI WA MAISHA BORA UNAONEKANA HATA KWA WATOTO WADOGO



**SAFARI MOJA HUANZISHA NYINGINE.KWANI MLIPONICHAGUA MLITAKA NIOTE
MATENDE IKULU?**

**MTOTO WA MZEE WA KAYA
CHAGUA MOJA KATI YA HIVI**

- (a) SHERIA**
- (b) FITNA JANGWANI**
- (c) USAIDIZI WA BABA**
- (d) SIASA CHAFU
YUVIISISIEM**

*HII BADO
INANICHANGANYA!
SIJUI
NI MINIMAIZ AU NI
KANSELI?*

*MH!
HATA HAELEWI
SOMO!*

©SAID
MICHAEL

**WE KATUNI HUELEWI SOMO LIPI TENA?YANI UNAKUWA KAMAMIE
NISIYEELEWA KWANINI TANZANIA NI MASIKINI!**



HAPANA.KOSA LA MSOMI HUYO WA CHUO KIKUU ANAYEFUKUZWA NA FFU NI KUGOMA KUCHUKUA HELA ZA KUJIKIMU ZILIZOINGIZWA KWENYE AKAUNTI YAKE KABLA HAJAWASILI CHUONI.HAPO ASKARI WA FFU ANAMHAMASISHA MSOMI HUYO AENDE BENKI.CHAGUA KIKWETE USOME KWA RAHA MUSTAREHE



**JIJENGE HUKO UVCCM.SI UMEONA FAMILIA YA BUSH ILITOA MARAIS WAWILI
KAMA YA KABILA HUKO DRC?BASI NA WEWE JIANDAE.MIE NAITWA CHAGUO
LA MUNGU,WEWE UTAITWA CHAGUO LA BABA**

!?

HII NDO TANZANIA
ZAIDI YA
UJUANYO..





**TATIZO LENU WATANZANIA MNA KUMBUKUMBU HAFIFU.MMESAHAU ENZI ZA
Boyz Il Men?MIE NA JAKAYA HATUJAFAHAMIANA MTAANI.MNABISHA?SI
MMEONA JINSI MAJUZI ALIVYOMWAGIA SIFA JIMBONI MONDULI?**



MAISHA BORA KWA KILA MTANZANIA YAMEWEZEKANA



MAJI BWERERE



**HUYU SLAA ANATAKA KUNIWEKEA MCHANGA BADALA YA UBWABWA
KWENYE SAHANI HII.HIZI HABARI ZA MIE KUFUKUZWA UALIMU ZA NINI TENA
MUDA HUU?**



**WANAKUJA NA USHAHIDI NINI?WANATOKEA HUKU AU
KULE?ANYWAY,HAWAWEZI KUTHIBITISHA LOLOTE**



**MGOSI,UNAKUMBUKA SIKU ZILEEEE KATIKA SHULE ILEEE...BASI SLAA
KAINYAKA HIYO ISHU.**



CHAGUA KIKWETE NA CCM KWA BARABARA BORA.NA 2010-2015 BARABARA KAMA HIYO HAPO JUU ZITAKUWA UPGRADED TO FLYOVER.



**BARABARA ZETU NI MARIDADI.TUMELETEWA MATREKTA MENGI MNO KWA
KILIMO KWANZA HADI INABIDI YAFANYE KAZI YA KUVUTA
MALORI.EBO!KWANI CHA AJABU NINI TREKTA KUVUTA LORI?NI FERI ZA NCHI
KAVU HIZO**



MNAONA?POLISI WENYE MAKAZI DUNI SASA WANA SWIMMING POOL HAPO MSIMBAZI POLICE FLATS.MAISHA BORA KWA POLISI YAMEPELEKEA WAACHE KUDAI RUSHWA NA KUBAMBIKIZA KESI KWA WALALAHOI



**MWAKYEMBE NA TUME YAKE NI ROHO MBAYA TU.KAMA MUME WANGU
LOWASSA ALIHUSIKA NA UFISADI WA RICHMOND MBONA KIKWETE AMEKUJA
JIMBONI KUMPIGIA DEBE?**



**TEH TEH TEH,NICHEKE MIE.KIKWETE MTU BOMBA SANA.SIE TUMEKUJA NA
KABRASHA TUPU LEO HII TUNA MABILIONI KWENYE AKAUNTI.ASANTE
DOWANS KWA KUTURITHI,ASANTE KARAMAGI NA MSABAHA.ASANTE
WATANZANIA KWA KUMWAMINI KIKWETE.SI MNAONA SASA TATIZO LA
UMEME NI HISTORIA KAMA ALIVYOAHI CHAGUO LA MUNGU KIKWETE?**



MFANO HAI WA AMANI NA UTULIVU



**ZAPATERO ANAELEKEA KUSHANGAA: HIVI KAMA HUYO JAMAA ANA MAWAZO
YA HALI YA JUU KIASI HIKI KWANINI BADO NCHI YAKE NI MASIKINI?NO,HAPO
KIKWETE ANAHUBIRI KUHUSU CHANZO CHA UMASIKINI WA AFRIKA JAPO
HAFHAMU KWANINI TANZANIA NI MASIKINI**



**MNASEMA NASAFIRI SANA?KWANI MLIPONICHAGUA MLIKUWA HAMFAHAMU
KUWA NILIPOKUWA WAZIRI WA MAMBO YA NJE NILIKUWA NASAFIRI
SANA?ACHENI UZUSHI,SAFARI ZANGU ZITAILETEA TANZANIA SIFA YA
KUVUNJA REKODI YA VASCO DA GAMA.**



**MMENG'ANG'ANIA TU SUALA LA EPA NA KAGODA NA KUSAHAU MINARA
PACHA.BY THE WAY,FEDHA ZA EPA HAZIKUIBWA BALI ZILIAZIMWA TU,NDIO
MAANA NILIWASIHI TULIOWAAZIMA WAZIREJESHE.WALIOAZIMWA
WANAREJESHA IN KIND KWA KUCHANGIA KAMPENI ZA CCM**



**TATIZO LA USAFIRI KWA WANAFUNZI MIJINI LIMEMALIZWA.MNATAKA MAISHA BORA
YAPI ZAIDI YA HAYA?**

**Nyie vijana hizo pesa
mnazonihoji mbona ni
VIJISENTI TU??? Kila kiongozi
ana viwango vyake.**





**KURA ZA ALBINO ZIMEZAA MATUNDA.HUYO MGOMBEA WA CCM WANAYEDAI
NI MTUHUMIWA WA BIASHARA YA VIUNGO VYA ALBINO NI SIASA ZA MAJITAKA
TU**



BAADA YA MABILIONI YA KIKWETE, NA KAGODA KUREJESHA MABILIONI, SASA MAISHA BORA NI KWA MWENDO WA PIPI KWA KILA MTOTO. YAH, PIPI KWANZA KISHA LAPTOP KWA KILA MWANAFUNZI. HALAFU HUYO SLAA ANAPOSEMA ATATOA ELIMU YA BURE KWANI MIE NAUZA HIZI PIPI?

Mwaka 2015 itakuwa je?

	2005	2010
Kiberiti	25	50
Unga	350	700
Mchele	650	1400
Sukari	650	1600
Cementi	5500	12500
Bati	6000	13000

Ee KIKWETE Uliye tufilisi, Jina lako USANII
MTUPU, utakalo lifanyike BAGAMOYO TU,
utupe leo mabilioni yetu ya EPA, uwapeleke
MAFISADI wote Mahakamani, uwape
WASTAAFU pesa zao, uwasamehe wafungwa
hasa BABU SEYA kama ulivyomsamehe
LOWASA, Usitutie katika mikataba FEKI, kwa
kuwa UFISADI ni fani yako na uwongo hata
milele, na Uanguke kwenye uchaguzi ujao
kama unavyoanguka hovyoyukwaani...

“AMINA”

Tanzania yenye neema inawezekana changua mabadiliko – Changua CHADEMA

www.wilbrodsla.com